**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam**
**Tarehe 28 Julai 2007**

**Waliohudhuria**
Ally Saidi Mohamedi
Ally Salum
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Hamadi Hatibu Bwaja
Juma Ali Salehe Jongo
Kassim Bakari
M. S. Mwenguo
Patrick Maziku
Paulo Atibu Hatibu
Rashidi Saidi Karanji
Sudi Saidi

Bwana Mwenguo ambaye ni mwenyekiti wa mtaa wa Jitegemee ambako UWABA inataka kuweka ofisi ilikaribishwa na kushukuriwa kwa msaada wake kufanikisha ufunguzi wa akaunti ya benki. Kwa vile anatumia baiskeli, alijiunga na UWABA>

**Sanduku la barua**
Iliamauliwa kufungua sanduku la barua la UWABA. Hata hivyo tunahitaji kuangalia sanduku la kaka yake Mejah kwani anuani hiyo ilitumika mara nyingi. Juma alisema atafuatilia posta ili kujua ni nini kinahitajika kabla ya kufungua sanduku.

**Ofisi**
Juma aliarifu kuwa fedha ya kodi imelipwa kutumia michango yote iliyopokelewa, amewekeana mkataba na kuchukua risiti.
Elaine aliarifu kuwa IBike imeahidi kuchangia Tsh 400,000 kama gharama za kuanzisha ofisi, kununua guta na kwa kodi ya baadae. Alikubaliana na David wa IBike aliyesema baadhi ya watu watafanya ziara na watapita Dar es Salaam mchana siku ya 31 Julai (Jumanne) na watakutana nasi na kutupatia mchango huo. Hata hivyo hakuweza kupata maelezo ya kutosha jinsi ya kuwasiliana nae au mahali pa kukutana nao. Atakapowapata atawatumia wajumbe wengine ujumbe.

**Kufungua ofisi**
Ilikubalika kuwa kwanza tutatakiwa kupaka rangi kuta zote kwani zilikuwa chafu sana, kupata rafu ili kuweka nyaraka dawati, baadhi ya viti/ mabenchi na baadhi ya mbao za matangazo na kitasa cha mlango. Baadae kama fedha zitatosha tutachora picha ya nembo yetu, baiskeli kwenye mlango na kuweka dari. Hamadi na Ally Saidi Mohamadi alisema watajitolea kupaka rangi na kutengeneza samani kama wakipata vifaa, kwani wote ni maseremala wazuri. Ilisemekana kuwa rangi itagharimu Tsh 10,000 na brashi ni Tsh 5,000. Ally saidi Mohamadi alisema atatafiti gharama za vifaa kwa utengenezaji  wa samani.

Elaine alizungusha picha ya baiskeli ya tairi tatu "smarty Hardy. Wanachama waliipenda lakini walidhani kwamba guta la kwaida lina soko zaidi kwa kukodisha kwani linabeba bidhaa zaidi. Ilikubalika kununua guta ikiwa tutapata mchango toka IBike au vyanzo vingine.

Sudi Saidi alisema kuwa anamfahamu meneja wa kampuni ya Gurudumu inayotengeneza baiskeli anayeitwa Bwana Ngaja. Alisema atakwenda Jumamosi hivyo Elaine alipiga simu ofisini na kuongea nae na kupanga mkutano jumatatu asubuhi saa 4 maeneo ya keko. Ilikubalika kama yupo mwanachama watakaotaka kuhudhuria watakutana kigogo round about saa 2 asubuhi Jumatatu , au kama wataweza waende moja kwa moja. Ilikubalika kwamba

a) tutaomba kupunguziwa gharama za guta na
b) tutafuatilia barua za kuomba mchango kwa msafara wa baiskeli.

**Msafara wa Baiskeli**
Elaine aliwasiliana na Bwana Nyoni ikiwa ITDP inaweza kuchangia msafara wa baiskeli na alisema labda – Elaine anajaribu kufuatilia kuhusu hili. Hakupatikana kuja kwenye mkutano kwani yuko Morogoro kwa sasa.

Elaine alifuatilia kwa simu na barua pepe na Bkhresa na Kinight Support ili kupata mchango kwa ajili ya msafara. Wote walisema wangepitia barua na Elaine afuatilie wiki ijayo.

Elaine alipeleka barua ambayo ilikubalika kuandaliwa wiki iliyopita kwa ajili ya mkutano na Azan Zungu mbunge kwa kupanda baiskeli na picha yake kutolewa kwenye gazeti na kumwomba kuwa mgeni rasmi kwenye msafara wa baiskeli. Juma alisema ataipeleka barua hiyo.

**Barabara zilizo kwenye mpango wa ujenzi**
Elaine alifuatilia TANROAD Dar es Salaam na makao makuu kuhusu barua zetu. TANROAD Dar es Salaam walisema hawajaona barua (ingawa Juma alisaini alipoifikisha hapo). Hivyo aliwatumia barua pepe. Makao makuu ya TANROADS walisema wamewapa CPC kujibu kwa upane wa barabara ya kilwa (na ilijibiwa). Kwenye barabara nyingine kwa ushirikiano kwa baadae walishauri tuonane na bwana Nitti, meneja wa maendeleo ili kuandaa mkutano wa kujadili mahitaji yetu. Bwana Nitti hakuwepo hivyo Elaine atapiga simu wiki ijayo.

**Wamba Memorial Fund**
Elaine alisema amepata mfuko uitwao wamba Memorial fund unatoa dola hadi 5,000 kwa mradi wa kukuza usalama barabarani. Pendekezo la mradi kupelekwa mwisho ni tarehe 31 August mahitaji yanajumuisha utaalamu na uzoefu wa kufanya miradi ya usalama barabarani ambapo UWABA haina, hivyo itakuwa vizuri ikiwa UWABA itatafuta mshirika mwenye ujuzi. Paulo alisema anafahamu shirika moja lililoko Ilala liitwalo UWATA ambalo wana ujuzi na uzoefu wa mambo ya usalama barabarani. Alisema atafuatilia kupata maelezo zaidi kuwahusu na kutufahamisha.

**Mengineyo**
Wanachama zaidi walichukua vitambulisho vyao na kutoa Tsh 500 kwa gharama za utengenezaji.

Jumanne alitupigia simu kututaka tupige picha guta lililokuwa nje ya ofisi yake lililohusishwa na ajali na kuharibiwa vibaya.

Kulikuwa na mjadala kuhusu wapanda baiskeli walioko Temeke, kwamba hawapo kwenye UWABA kwa sababu ofisi yetu iko mbali nao. Ilikubalika kuwa wakati ujao tuwe na ofisi kila wilaya.